



LIALE FARM ESTATE COMPANY LIMITED

KIKAO CHA BODI YA WAKURUGENZI 12/11/2021

AGENDA

- KUFUNGUA KIKAO
- MAENDELEO YA ZAO LA KAHAWA
- TAARIFA MBALIMBALI
- KUOMBA USAJIRI KWENYE TANZANIA INVESTMENT CENTRE (TIC)
- MENGINEYO
- KUFUNGA KIKAO

MAHUDHURIO:

1. Said Mussa Banda - mwenyekiti
2. Elizabeth Mapunda - katibu
3. Godfrey K Nditi - mjumbe
4. Arnold Haule - mjumbe
5. Rashid Banda - mjumbe


.....

.....

.....

.....

.....

KUFUNGUA KIKAO

Mwenyekiti alifungua kikao saa 5.30 asubuhi kwa kuwakaribisha wajumbe kwa kuwaomba wawe watulivu katika kikao hiki cha kiutendaji kwa kihitimisha mwaka kimkakati.

MAENDELEO YA ZAO LA KAHAWA

Mwenyekiti aliwataarifu wajumbe kwamba shamba letu la kahawa lilioko LIHALE linaendelea vizuri sana kwani hata mavuno yake yanatia hamasa ingawa vitendea kazi vinatatiza kulingana na hali halisi ya uchumi. Hivyo inatulazimu kuboresha shamba hilo ili tupate mavuno mengi pia tutengeneze kama shamba la mfano kusudi wakazi wanaozunguka shamba waje kujifunza na kujipatia ajira. Katika msimu huu wa mavuno tuli8fanikiwa kupata zaidi ya tani 135 ambazo

zimekoborewa kwenye kiwanda cha CMS-Mbinga kisha kuuzwa mnadani baada ya kupata kibali toka TANZANIA COFFEE BOARD. Mwenyekiti alizidi kufafanua kwamba shamba linahitajika kupanuliwa zaidi kwani zimeendelezwa kiasi kidogo sana hasa eneo tulilopata hatimiliki na eneo lingine bado kabisa na linahitajika kuendelezwa na kupatiwa hatimiliki nyingine kwa mujibu wa sheria za Ardhi na sheria ndogondgo za kijiji .

TAARIFA MBALIMBALI

Mwenyekiti alitoa taarifa kwamba shamba letu ni moja ya mashamba madogo nay a kati (min estate) zilizoko mkoani Ruvuma na inatulazimu tufuatilie katika taasisi za serikali ili tupate uwezo wa kuliboresha la sivyo sisi wenyewe hatutaweza kufikia malengo mapema, pia mwenyekiti alitoa taarifa kwamba uongozi wa halmashauri na bodi ya kahawa unatoa ushirikiano mkubwa kwa ushauri wa kitaalamu dhidi ya kuendesha shamba . Hivyo Mpango mkakati wa kuboresha shamba ufanyike kwa kujenga miundo mbinu ya kilimo cha umwagiliaji.

KUOMBA USAJIRI KWENYE T. I. C.


Mwenyekiti aliwaeleza wajumbe juu ya umuhimu wa kuomba usajiri kwenye Tanzania Investment Centre kusudi shamba letu lipate kibali kama wawekezaji wazalendo tulisubutu kuonyesha nia ya kuendeleza kilimo cha zao la biashara la kahawa. Inatupasa kufuata utaratibu wa serikali katika kujisajiri ili shamba liwe mmojawapo la mfano kwa wazao kuendesha kilimo cha tija, katika kufanya hivyo wakurugenzi wenzangu wa bodi tukubaliane nami katika kupitisha muhtasari huu ili hatua inayofuata iendelee. Wajumbe waliunga mkono wazo hilo ila walitoa angalizo kwamba tuwe makini kusudi iwe rahisi katika kufanya usajiri . Wazo hili lililopita bila kupingwa na kikao kizima. Hivyo kikao kiliwaagiza uongozi wafanye haraka utaratibu huo ili kusudi kuendana utaratibu wa serikali katika kusajiri shamba letu .

MENGINEYO.

Hakuna mengineyo iliyokuwepo kwa vile wajumbe hawakuwakuleta mapema kwenye agenda.


KUFUNGA KIKAO.

Kikao kilifungwa saa 8.00 mchana kwa kuwashukuru wajumbe kwa mawazo yao ya kujenga aliomba tuendeleze mshikamano katika mapambano haya ya kiuchumi.



Sahihi ya mwenyekiti

Tarehe 14/11/2021



Sahihi ya katibu

Tarehe 14/11/2021

